**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**

# TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOFUNGULIWA, KUZINDULIWA NA KUWEKEWA MAWE YA MSINGI NA KIONGOZI WA MBIO ZA

# MWENGE WA UHURU

# 3 SEPTEMBA 2017

**Septemba, 2017**

## UTANGULIZI

Kitabu hiki kinahusu taarifa mbalimbali za mbio za Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha tarehe 3 Septemba 2017. Aidha, taarifa hizo ni pamoja na Taarifa ya Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru, Mapokezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Ratiba za Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru, Taarifa za Miradi, Risala ya Utii kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Taarifa ya Kuukabidhi Mwenge kwa Halmashauri ya Meru, na viambatanisho muhimu vya vya taarifa hizo.

**TARIFA FUPI YA MAKABIDHIANO YA MWENGE**

**TAREHE 3 SEPTEMBA 2017**

Mimi **Ndugu Alexander Mnyeti**, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, nakiri kuupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Longindo, leo tarehe **3 Septemba 2017** ukiwa unawaka, unameremeta na wakimbiza Mwenge kimkoa na Kitaifa wakiwa na afya njema na salama.

Katika Wilaya ya Arumeru inayoundwa na Halmashauri mbili, **Halmashauri ya Wilaya ya Arusha** na **Halmashauri ya Meru.** Wilaya ya Arumeru ina ukubwa wa kilomita za mraba **2,714.892** ikiwa na jumla ya Wakazi **663,055** **(**Wanaume ni **319,690)** na Wanawake ni **343,096).** Aidha, Mwenge wa Uhuru utapita katika Tarafa zote **6** za Wilaya ambazo ni **Mukulat, Enaboishu, Moshono, King'ori, Poli** na **Mbuguni**, utapita katika kata **10** kati ya kata **53**, vijiji **8** kati ya **157**.

Mwenge huu wa Uhuru unatarajiwa kukimbizwa umbali wa Kilometa **159.1** kukagua na kufungua miradi yenye thamani ya shillingi **3,735,799,088** katika Sekta za Maji, Elimu, Afya, Viwanda, Uvuvi, Kilimo, Mazingira na Mifugo na kuwezesha wananchi kiuchumi hasa kwa kutoa mikopo kwa vikundi yenye thamani ya shilingi **157,000,000.**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa kwa kuanzia Mwenge huu wa Uhuru utaanza kukimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na kumalizikia katika Halmashauri ya Meru.

Eeeh Mwenyezi Mungu nisaidie.

**Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!**

Ndugu Alexander Mnyeti
**MKUU WA WILAYA**
**WILAYA YA ARUMERU**

## TAARIFA FUPI YA MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU TAREHE 03 SEPTEMBA 2017

**UTANGULIZI**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, **Amour Hamad Amour**, Ndugu wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa ; Salome Obadia Mwakitalima, Shukran Islam Msuri, Frederick Joseph Ndahani, Vatima Yunus Hassan, Bahati Mwaniguta Lugodisha,

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha - Ndugu Mrisho Gambo

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha - Ndugu Richard Kwitega

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru – Ndugu Alexander Mnyeti

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama na Serikali

Viongozi wa Madhehebu ya Dini

Viongozi wa Tasnia ya habari, vikundi vya wasanii

Kwa niaba ya wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha napenda nitumie fursa hii kuwapa pole kwa safari ndefu. Aidha, ninayo furaha kubwa kuwakaribisha katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Sote tunatambua kwamba kihistoria, **Mwenge wa Uhuru uliwashwa ili kuleta matumaini pasipo na matumaini, kuleta upendo palipo na chuki, na heshima pale ambapo pamejaa dharau.** Hadi sasa, pamoja na kuhimiza maendeleo kwa wananchi, Mwenge wa Uhuru bado unabeba maana na madhumuni yale yale yaliyoainishwa wakati Mwenge wa Uhuru unawashwa kwa mara ya kwanza nchini.

Katika kutekeleza madhumuni hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, yenye Jimbo moja la uchaguzi la Arumeru Magharibi, Mwenge wa Uhuru utapita katika Tarafa zote **tatu (3)** ambazo ni **Mukulat, Enaboishu** na **Moshono.** Aidha, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Kata **Sita (6)** kati

ya kata **27** na utapita katika vijiji **vinne (4)** kati ya Vijiji **67** na vitongoji **vinne (4)** kati ya vitongoji **21** vinavyounda Mamlaka ya Mji mdogo wa Ngaramtoni katika Halmashauri hii.

Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017 katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha zitakuwa na urefu wa kilomita **88.** Mwenge wa Uhuru utapitia miradi **sita (6)**, kati ya hiyo miradi **miwili (2)** itafunguliwa nayo ni Kituo cha Afya Engorora kilichopo Kata ya Kisongo na mradi wa ufugaji wa samaki, uliopo Kata ya Olorien. Miradi **mitatu (3)** itazinduliwa nayo ni mradi wa Kiwanda cha vifungashio uliopo Kata ya Kisongo, Mabweni na madarasa shule ya Sekondari Mwandet, uliopo Kata ya Mwandet na Kivuko cha Moivo kilichopo Kata ya Moivo. Na mradi **mmoja (1)** wa maji wa Ekenywa, Kata ya Olturument utawekewa jiwe la msingi na Mwenge wa Uhuru. Aidha, Mwenge wa Uhuru utatekeleza dhana ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi na kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na Vijana yenye thamani ya shilingi **100,000,000.**

Miradi yote hii ina thamani ya jumla ya Shillingi **1,635,900,399.45** kwa mchanganuo ufuatao : -

| Nguvu za Wananchi | Halmashauri | Serikali Kuu | Wadau wa Maendeleo |
|---|---|---|---|
| 163,350,700.00 | 80,849,699.45 | 255,000,000.00 | 1,136,700,000.00 |

Miradi itakayopitiwa imegusa sekta za Maji, Elimu, Afya, Viwanda, Uvuvi, na kuwezesha Wananchi kiuchumi.

Pamoja na kupitia miradi ya maendeleo, Mwenge wetu wa Uhuru utakimbizwa ukiwa unaelimisha na kueneza ujumbe mkuu wa ***'Shiriki kukuza Uchumi wa Viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu'.*** Aidha ujumbe

huu umeambatana na ujumbe wa kudumu wa mapambano dhidi ya Malaria, UKIMWI, Rushwa na matumizi ya madawa ya kulevya.

**Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha imejiandaa vyema kuupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru kwa shangwe, nderemo, bashasha na vifijo ikiwa ni pamoja na kuangalia vyema msafara wako. Hivyo ninayo heshima kubwa kutamka sasa kuwa tuko tayari kuanza mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017.

**MWENGE HOYEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEEE !!!!!!!!!**

Dkt. Wilson Mahera Charles (PhD)
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI WILAYA YA ARUSHA**

**RATIBA YA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2017**

**03.09.2017 NA 04.09.2017**

**SIKU YA KWANZA TAREHE 03.09.2017**

| KATA | ENEO | MUDA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Oldonyowass | Ofisi ya Kata Oldonyowas | 12:00-2:00 | Kuwasili eneo la Mapokezi | Viongozi Wananchi |
| Oldonyowass | Ofisi ya Kata Oldonyowas | 02:00-2:15 | Watumishi na wananchi Kujipanga tayari kwa Kuupokea Mwenge wa Uhuru. | Viongozi Watumishi Wananchi |
| Odonyowass | Ofisi ya Kata Oldonyowass **0km** | 2:15-2:50 | Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru | Mkuu wa Wilaya ya Longido na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. |
| Oldonyowass | Ofisi ya Kata Oldonyowass **0km** | 2:50-3:00 | Wimbo wa kuukaribisha Mwenge | Kikundi cha Halaiki na amsha amsha. |
| Olturument | Ekenywa **20.6 Km** | 03:00-3:15 | Mwenge wa Uhuru kuwasili Kijiji Cha Ekenywa. | OCD Mkuu wa Wilaya |
| | | 03:15-3:30 | Kuweka Jiwe la Msingi kwenye mradi wa maji Ekenywa. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa. |
| Mwandet | Mwandet **8 Km** | 03:30-3:45 | Mwenge wa Uhuru kuwasili Shule ya Sekondari Mwandet. | OCD Mkuu wa Wilaya |

| KATA | ENEO | MUDA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| | | 03:45-4:00 | Kuzindua Bweni la wasichana Shule ya Sekondari Mwandet. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| | | 04:00-04:15 | Kufungua Madarasa Shule ya Sekondari Mwandet. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| | | 04:15-4:45 | Ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| | | 4:45-4:55 | Igizo/Ngonjera kuhusu Rushwa | Wanafunzi Mwandet Sekondari |
| | | 04:45-5:15 | Chai ya asubuhi. | Watu wote |
| Kisongo | Kituo cha Afya Engorora **23km** | 05:15-05:45 | Mwenge wa uhuru kuwasili kituo cha afya Engorora. | OCD<br>Mkuu wa Wilaya |
| | | 05:45-06:00 | Kufungua kituo cha Afya Engorora | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| Kisongo | Lovilukunyi **7Km** | 06:00-06:20 | Mwenge wa Uhuru kuwasili katika Kiwanda cha kutengeneza vifungashio. | OCD<br>Mkuu wa Wilaya |
| | | 06:20-06:35 | Kuzindua Kiwanda | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| Olorien | Eneo la Mradi **30Km** | 06:35-07:00 | Mwenge wa uhuru kuwasili eneo la Mradi | OCD<br>Mkuu wa Wilaya |
| | | 07:00-07:15 | Kufungua mradi wa samaki. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |

| KATA | ENEO | MUDA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Moivo | Shule ya Sekondari Ilboru **6Km** | 7:15 -7:25 | Mwenge wa Uhuru kuwasili Ilboru Sekondari | OCD Mkuu wa Wilaya |
| | | 07:25-08:05 | Ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru. | Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa |
| | | 08:05-09:25 | Chakula cha Mchana | Watu wote |
| Moivo | Moivo **2Km** | 09:25-09:35 | Mwenge wa Uhuru kuwasili. | OCD/ Mkuu wa Wilaya |
| | | 09:35-09:50 | Kuzindua daraja La Moivo. | Kiongozi Wa Mbio Za Mwenge Wa Uhuru |
| Kiutu | Kiutu **3Km** | 09:50-11:30 | Mwenge wa Uhuru kuwasili eneo la mkesha. | OCD/ Mkuu wa Wilaya |
| | | | Kutoa Mikopo kwa Vikundi vya vijana na wanawake | Kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa |
| | | | Kutembelea miradi ya vikundi inayotekeleza dhana ya viwanda | Kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa |
| | | | Kutembelea banda la upimaji UKIMWI/VVU | Kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa |
| | | | Kusoma risala ya utii kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. | DAS/DED |
| | | | Kutambulisha wakimbiza Mwenge Kimkoa na Kitaifa. | Kiongozi Wa Mbio za Mwenge Wa Uhuru |

| KATA | ENEO | MUDA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| | | | Ujumbe Wa Mwenge Wa Uhuru | Kiongozi Wa Mbio Za Mwenge Wa Uhuru |
| | | 11:30-01:30 | Shairi, Kwaya, Igizo na burudani mbalimbali | Kikosi cha Sanaa, ACE Africa na JKT Oljoro |
| Kiutu | Viwanja vya Halmashauri | 01:30-02:30 | Chakula cha Usiku. | Wote |
| Kiutu | Viwanja vya Halmashaur | 02:30-12:30 | Mkesha wa Mwenge na burudani mbalimbali | Wote |
| **SIKU YA PILI TAREHE 04.09.2017** | | | | |
| Kiutu | Viwanja vya Halmashauri | 12:30-2.00 | Chai ya asubuhi | Wote |
| Kiutu | Viwanja Vya Halmashauri | 2:00-2:30 | Msafara Kuelekea Tengeru eneo la makabidhiano | OCD/ Mkuu wa Wilaya |
| H/shauri ya Meru | Soko la Tengeru **9.5 Km** | 2:30-9:00 | Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru | Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Meru |

## MRADI I

## TAARIFA YA MRADI WA MAJI KITONGOJI CHA EKENYWA.

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa. Mradi wa maji kitongoji cha Ekenywa katika Kata ya Olturumet ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa katika Halmashauri yetu kwa fedha za Mapato ya Ndani (Fedha ya fidia shamba la Lakilaki) na Ruzuku kutoka Serikali Kuu (CDG). Mradi huu uliibuliwa na wananchi kutokana na tatizo la maji katika maeneo yao ambapo maji hupatikana mara mbili kwa wiki na umbali wa kufuata maji ni zaidi ya mita **400**. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Juni 2017 na wataalam wa idara ya maji kwa kushirikiana na wananchi wa kitongoji cha Ekenywa. Mradi umelenga kujenga tanki la Maji lenye mita za ujazo **60**, ulazaji wa bomba la usambazaji na bomba kuu umbali wa kilometa **13.15** ambapo kilomita 10 ni bomba la usambazaji na kilomita **3.15** ni bomba kuu. Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji **15** pamoja na ujenzi wa uzio (Chainlink fence).

Kazi zilizofanyika ni pamoja na; Ujenzi wa tanki lenye **mita za ujazo 60** umefanyika kwa **asilimia 95** na ulazaji wa bomba kuu kilometa **3.15** umekamilika.



**Picha Na 1:** ***Tanki lenye mita za ujazo 60 mradi wa Maji Ekenywa***

**GHARAMA ZA MRADI**

Mradi huu ulipofikia hadi sasa umegharimu jumla ya shilingi **58,448,099.45.** Gharama ya mradi imejumuisha nguvu za Wananchi na mchango kutoka Serikalini. Mchanganuo ni kama ufuatao: -

| | |
|---|---|
| Nguvu za Wananchi | Shilingi 10,500,000 |
| Ruzuku toka Serikali kuu (CDG) | Shilingi 25,000,000 |
| Halmashauri | Shilingi 22,948,099.45 |
| **Jumla** | **58,448,099.45** |

Hadi kukamilika mradi huu unakadiriwa utagharimu jumla ya shilingi **150,948,099.45/=.**

**MANUFAA YA MRADI**

Mradi huu ukikamilika unatarajiwa: -

1. Kuhudumia wananchi wapatao 3,750 wa kitongoji cha Ekenywa hivyo kupunguza tatizo la kufuata maji umbali mrefu unao athiri shughuli za uzalishaji mali.
2. Kuhudumia Hospitali ya Olturument, Shule ya Msingi pamoja na Sekondari,
3. Kupunguza umbali wa Wananchi kupata maji safi na salama katika maeneo wanapoishi.

**HITIMISHO**

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Serikali ya Kitongoji cha Ekenywa, Wananchi, Halmashauri ya Wilaya Arusha na wadau wote waliofanikisha ujenzi wa mradi huu. Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa, tunaomba utuwekee jiwe la Msingi katika mradi huu wa Maji Ekenywa.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!**

Anna Kivuyo
**AFISA MTENDAJI WA KATA**
**KATA YA OLTULUMENT**

**MRADI II**

**TAARIFA YA MRADI WA BWENI LA KIDATO CHA TANO NA SITA**

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi huu wa ujenzi wa bweni la Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Mwandet ulianza rasmi mwezi Aprili mwaka 2017. Mradi umefadhiliwa wa Serikali kuu kupitia mradi wa **Lipa kulingana Matokeo "Payment for Results" (P4R)** pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ikishiriki katika usimamizi wa mradi.

Mradi umelenga kuboresha miundombinu ya malazi bora kwa Wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita wa shule hii. Bweni hili lina uwezo wa kuhudumia wanafunzi wapatao **80**.



**Picha Na. 2:** ***Bweni la Shule ya Sekondari Mwandet***

**GHARAMA ZA MRADI**

Hadi kukamilika mradi huu wa ujenzi umegharimu kiasi cha shilingi **174,298,200/=.**

Mchanganuo wa fedha ni kama ifuatavyo Fedha kutoka serikali kuu kupitia mradi wa P4R shilingi **150,000,000** na Nguvu za Wananchi **24,298,200**.

**MANUFAA YA MRADI**

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, mradi huu umekuwa na manufaa makubwa yafuatayo: -

- Kuwezesha ubora wa elimu hasa kwa wanafunzi wakike kwa kuishi karibu na shule,
- Kuongeza nafasi za wanafunzi wa kidato cha tano,
- Kuongeza kiasi cha ufaulu kwa kuwa na wanafunzi wanasoma kwa ushirikian na kusaidiana,
- Kuongeza mwamko wa Elimu kutokana na wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali Tanzania,
- Bweni limesaidia wanafunzi kuwa na muda mwingi wa kujisomea kwa pamoja.

**HITIMISHO**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa tunaomba utuzindulie Bweni hili la Shule ya Sekondari ya Mwandet.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!**

Mwalimu John Massawe
**MKUU WA SHULE**
**SEKONDARI MWANDET**

**MRADI III**

## TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VINNE VYA MADARASA

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi huu wa ujenzi wa Madarasa manne ya kidato cha Tano na Sita katika Shule hii ya Sekondari ya Mwandet ulianza rasmi Mwezi Aprili mwaka 2017.

Mradi huu umefadhiliwa na Serikali Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mradi wa **Lipa kulingana Matokeo "Payment for Results" (P4R)** na ukisimamiwa na wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Madarasa haya yana uwezo wa kuhudumia wanafunzi wapatao **160**.



**Picha Na 3:** ***Madarasa ya kidato cha tano na sita katika shule ya Sekondari Mwandet***

## GHARAMA ZA MRADI

Hadi kukamilika mradi huu wa ujenzi umegharimu jumla ya shilingi **88,552,500** ikiwa ni mchango kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa P4R shilingi **80,000,000** na Nguvu za Wananchi shilingi **8,552,500**.

**MANUFAA YA MRADI**

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, mradi huu umekuwa na manufaa yafuatayo; -

- Wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne kuweza kupata nafasi kujiunga na masomo ya kidato cha tano na sita.
- Kuboresha miundombinu yakujifunzia kwa wanafunzi wa kidato cha Tano na Sita.
- Kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani hasa kwa wanafunzi wa "A level".
- Kuongeza wa udahili wa wanafunzi hasa wa kidato cha tano na sita,
- Imepunguza mzigo wa ujenzi wa madarasa kwa wananchi na Halmashauri.

**HITIMISHO**

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa tunaomba utuzindulie madarasa haya.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!**

Mwalimu John Massawe
**MKUU WA SHULE**
**SEKONDARI MWANDET**

## MRADI IV

## TAARIFA YA MRADI WA KITUO CHA AFYA ENGORORA

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi wa Kituo cha Afya Engorora uliwekwa jiwe la msingi na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2016 aliyeitwa **Ndugu George Jackson Mbijima**.

Lengo kuu la mradi huu ni kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Hii ni sambamba na utekelezaji wa sera ya Afya inayotaka kuwepo kwa huduma za Afya karibu na katika kila Kijiji.



**Picha Na 4:** ***Kituo cha Afya Engorora, katika Kata ya Kisongo.***

## GHARAMA ZA MRADI

Hadi mradi huu ulipofikia umegharimu jumla ya **Tsh. 151,501,600** ikiwa ni nguvu za wananchi na mchango kutoka Serikalini kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Nguvu za Wananchi | Shilingi 120,000,000 |
| Wahisani/Wadau wa Maendeleo | Shilingi 8,000,000 |
| Halmashauri | Shilingi 23,501,600 |
| **Jumla** | **Shilingi 151,501,600.00** |

Hadi kukamilika mradi huu kama unavyoonekana umegharimu jumla ya shilingi 151,501,600.

**MANUFAA YA MRADI**

Ni pamoja na

- Mradi huu unakadiriwa kuhudumia wananchi takribani **10,365** wa Kata ya Kisongo na baadhi ya vijiji vya Kata za jirani.
- Kutoa huduma za afya pamoja na upimaji wa UKIMWI/VVU,
- Kupunguza vifo vya watoto na wamama wajawazito kwa kusogeza huduma karibu na Jamii,
- Kutimia kwa azma ya Serikali ya kutaka kila Kata kuwa na kituo cha Afya, Kata hii ya Kisongo imetimiza.
- Kutimia kwa lengo namba 3 linalohusu afya njema (Good Health) la Maendeleo Endelevu 2030 (Sustainable Development Goals).

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa, tunaomba utufungulie kituo hiki cha Afya cha Engorora.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!**

James A Shore
**AFISA MTENDAJI WA KATA**
**KATA YA KISONGO**

## MRADI V

## MRADI WA KIWANDA CHA KUTENGENEZA VIFUNGASHIO (ACTIVE PACKAGING)

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi huu wa kutengeneza vifungashio aina ya mabox ulianza rasmi mwaka 2015 na kuanza uzalishaji mwaka 2017. Wazo la kuanzisha kiwanda hiki lilikuwepo kitambo kidogo lakini kutokana na urasimu mwingi hakikuweza kuanzishwa. Aidha utekelezaji ulianza **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli** alipoingia madarakani 2015 na kutangaza azma ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Uchumi wa Viwanda.

Lengo la Kiwanda hiki ni kutengeneza na kuuza vifungashio vya aina mbalimbali vya mabox kwa kutumia malighafi za hapa hapa nchini hivyo kusaidia kutoa ajira kwa vijana. Aidha, uzalishaji wa kiwanda ni tani 30 hadi 40 kwa mwezi.



**Picha Na 5:** *Kiwanda cha Vifungashio cha Kisongo (Active Packaging)*

## GHARAMA ZA MRADI

Mradi huu hadi kukamilika kwake umegharimu kiasi cha shilingi **950,000,000** ambazo shilingi **400,000,000** ni mkopo kutoka benki ya TIB, shilingi **550,000,000** ni fedha za Mmiliki wa mradi ndugu **Prosper Swatty**.

## MANUFAA YA MRADI

Mradi huu umefanikiwa kuwa na manufaa kama yafuatayo: -

- Mradi huu umetoa ajira kwa watu **10** wengi wao wakiwa ni vijana,
- Mradi huu pia umewezesha upatikanaji wa vifungashio bora kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, hivyo kukuza uchumi wa nchi.
- Uwepo wa kiwanda hiki ni soko kwa malighafi kutoka katika kiwanda cha Karatasi Mufindi, Iringa.
- Mradi huu ni rafiki kwa mazingira kwani unatumia nishati ya umeme katika uzalishaji wake. Na mabaki ya tokanayo na uzalishaji wa vifungushio yanauzwa Kenya, hata hivyo kuna mpango wa kuyatumia kwa hapo baadae kwa kufanya (recycling).
- Kutumia malighafi kutoka kiwanda cha karatasi Mufindi hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

## HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa tunaomba utuzindulie mradi huu.

**"Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu"**

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!**

Prosper Swatty
**MMILIKI WA KIWANDA**
**ACTIVE PACKING**

## MRADI VI

## TAARIFA YA MRADI WA SAMAKI- OLORIEN

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi wa ufugaji wa samaki wa Shamba la Trust Patrick ulianza rasmi mwezi **Machi, 2017** na kukamilika mwezi **Agosti, 2017** kwa shughuli za uchimbaji na ujenzi wa mabwawa mawili yenye uwezo wa kubeba vifaranga vya samaki **4000** kila Bwawa, hivyo kufanya jumla ya vifaranga **8000** kwa mabwawa yote **mawili (2)**.



**Picha Na 6:** ***Mabwawa ya kufugia Samaki Olorien***

### GHARAMA ZA MRADI

Hadi sasa mradi huu wa ufugaji wa samaki hadi kukamilika umegharimu jumla ya kiasi fedha shilingi **178,700,000.**

Kati ya hizo miundo mbinu ya maji imegharimu shilingi **46,000,000**, Ujenzi wa Mabwawa pamoja na vifaranga vya samaki umegharimu shilingi **49,700,000/=** na ujenzi wa uzio umegharimu shilingi **83,000,000/=**.

**MANUFAA YA MRADI**

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, mradi huu umekuwa na manufaa yafuatayo: -

- Mradi huu kutoa ajira kwa Vijana **11** kwa kuanzia,
- Pia mradi huu kusaidia utunzaji wa mazingira,
- Kuboresha Afya za Jamii kwa kujipatia lishe bora kwa kutumia samaki.
- Kuwa sehemu ya mfano kwa watu mbalimbali kujifunza kuhusu ufugaji wa samaki.

**HITIMISHO.**

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa kutoa mtaalamu wa Uvuvi **Ndugu Mfinanga H.A** aliyewezesha kutayarisha andiko la mradi, usimamizi, ushauri, na mafunzo ya muda mrefu.

Kwa kutekeleza sera ya Viwanda, tutaanza kufikiria kuwa na kiwandakidogo cha kusindika Samaki kwa hapo badae.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwa heshima na taadhima tunaomba utufungulie mradi huu,

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!!**

Mike P. Khanya
**MENEJA MSAIDIZI WA SHAMBA**
**TRUST PATRICK FISH FARM**

## MRADI VII

### MRADI WA UJENZI WA KIVUKO- KATA YA MOIVO

Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mradi huu wa ujenzi wa kivuko cha Moivo ulianza rasmi **Machi, 2017** na kumalizika Julai 2017 ukiwa na lengo la kuimarisha miundombinu Katika Halmashauri yetu hasa kwa wananchi wa Kata ya Moivo.

Mradi huu umekuja baada ya uchakavu wa kivuko cha awali kilichokuwa kikihatarisha usalama wa watumia kivuko. Fedha za mapato ya ndani Halmashauri ya Wilaya ya Arusha zimegharamia mradi huu.



**Picha Na 7:** ***Kivuko cha Moivo***

### GHARAMA ZA MRADI

Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi za kitanzania **40,000,000**, lakini hadi kukamilika kwa Mradi huu uligharimu jumla ya shilingi **34,400,000**.

Hivyo fedha iliyobakia kiasi cha shilingi **5,600,000** imeelekezwa kutatua changamoto za kimaendeleo zilizopo ndani ya kata husika ya Moivo.

**MANUFAA YA MRADI**

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, mradi huu umefanikiwa kuwa na manufaa kama yafuatayo:

- Mradi huu umeboresha usafiri ndani ya kata ya Moivo,
- Kuchochea Maendeleo katika Vitongoji vinavyounganishwa na kivuko hiki.

**HITIMISHO**

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge kitaifa, tunaomba utuzindulie Kivuko hiki cha Moivo.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!**

Dorah F Mollel
**AFISA MTENDAJI KATA**
**KATA YA MOIVO**

**RISALA YA UTII YA KWA RAIS**

**Mheshimiwa Rais,**

Sisi wananchi wa Halmashauri ya wilaya ya Arusha tunayo furaha kubwa kuungana na watanzania wengine leo tarehe **03 Septemba 2017** kuupokea na kuukimbiza **MWENGE WA UHURU** katika Halmashauri yetu. Aidha tunawakaribisha Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na kuwapongeza Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndugu **Salome Obadia Mwakitalima**, **Shukran Islam Msuri**, **Fredrick Joseph Ndahani**, **Vatima Yunus Hassan** na **Bahati Mwaniguta Lugodisha** chini ya Uongozi wa Ndugu, **Amour Hamad Amour**, kwa kazi kubwa wanayofanya mwaka huu.

**Mheshimiwa Rais,**

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ina ukubwa wa kilomita za mraba **1,446.692** na inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi wapatao **382,007** ambapo kati yao **Wanaume** ni **182,378** na **Wanawake** ni **199,629**. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ina Jimbo moja la uchaguzi la Arumeru Magharibi, Kiutawala kuna jumla ya Tarafa **3**, Kata **27**, vijiji **67**, vitongoji **256** na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni. Mwaka **2016** mwenge wa Uhuru ulikimbizwa kimkoa na Halmashauri yetu ilikuwa na miradi **saba (7)** yenye thamani ya shilingi **3,110,645,234** ambapo miradi **mitatu (3)** ilifunguliwa, miradi **miwili (2)** ilizinduliwa na miradi **miwili (2)** iliwekwa jiwe la msingi na kwa sasa miradi yote imekamilika na inatumika. Maendeleo ya Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru kwa miaka mitatu **2014**, **2015** na **2016** imeambatanishwa katika viambatisho vya risala hii ya utii.

**Mheshimiwa Rais,**

Katika utekelezaji wa dhana ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Halmashauri inayo **SACCOS moja** ya vijana ambayo inaendelea kujengewa uwezo. Aidha, uchaguzi unatarajiwa kufanyika ili kuondoa waliozidsha umri wa miaka **35**. Mwaka **2016/2017** Halmashauri imefanikiwa kuhamasisha na

kuunda vikundi **72** vya vijana vya uzalishaji mali vyenye wanachama **576** ambapo wasichana ni **212** na wavulana ni **364**, na jumla ya vikundi **221** vya wanawake vya uzalishaji mali vyenye jumla ya wanachama **3315**. Halmashauri ilitenga jumla ya **Tsh 114,240,635.42** kutoka katika mapato ya ndani na ilitoa Tsh. **196,500,000** kwa vikundi **16** vya vijana vyenye wanachama **154**, na vikundi vya wanawake **44** vyenye wanachama **612**. Shilingi **152,500,000** kwa Wanawake na shilingi **44,000,000** kwa vikundi vya Vijana.

Aidha, leo tumetoa mikopo yenye thamani shilingi **100,000,000** kwa vikundi **16** vya wanawake na vikundi **7** vya vijana. Halmashauri imekuwa na historia ya kutoa mikopo kwa vijana kama kwa miaka ya 2014, 2015 na 2016 kama ilivyo kwenye *Viambatanisho* vya taarifa za Miradi ya Mwenge wa Uhuru.

Halmashauri imetoa tenda ya usafi wa mazingira kwa kikundi kimoja cha vijana chenye wanachama wapatao **26** kiitwacho ASODEG Youth Group cha Kata ya Kiutu. Kwa upande wa ajira za vijana, takwimu zinaonyesha idadi ya vijana walioajiriwa katika sekta rasmi ni 426 na 6,762 katika sekta isiyo rasmi.

**Mheshimiwa Rais,**

Halmashauri, imefanya jitihada za kuunda timu ya Uwekezaji, kuandaa wasifu wa uwekezaji "Investment Profile" na kutangazwa kwenye tovuti ya Halmashauri www.arushadc.go.tz. Kuhamasisha wananchi kuanzisha viwanda. Hadi kufikia Juni 2017 Halmashauri ina jumla ya viwanda vya kati **17** na viwanda vidogo **241** vilivyotengeneza ajira **695**. Kuainishwa kwa maeneo ya ujenzi wa viwanda yapatayo matatu (3) ambayo ni Mbuga ya Ilkurot katika Kata ya Olkokola lenye ukubwa **ekari 50**, Shamba la Hifadhi Builder Ltd lililopo Kata ya Bwawani ukubwa **ekari 18**, Shamba la Oldonyosambu lenye ukubwa **ekari 20.** Maeneo yote matatu yana miundombinu wezeshi ya ujenzi wa viwanda. Aidha, katika kuhamasisha

sekta binafsi kuanzisha viwanda Halmashauri kwa kutumia mitambo yake imeboresha miundombinu ya barabara inayoelekea katika maeneo hayo. Pia, Halmashauri inatoa huduma na nyaraka mbalimbali kwa wakati kwa wawekezaji wa viwanda. Aidha, mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu 2017 umezindua kiwanda cha mtu binafsi cha kutengeneza vifungashio (Active Packing) katika kata ya Kisongo.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa mwaka huu wa 2017, **MWENGE WA UHURU** katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha umezindua, umefungua na kuweka mawe ya msingi. Jumla ya thamani ya Miradi hiyo ni shilingi **1,635,900,399.45** kwa mchanganuo ufuatao: -

**A. Miradi iliyozinduliwa Mitatu yenye thamani ya Shilingi 1,247,250,700**

| Na | Mradi | Kata | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Bweni la Wasichana pamoja na | Mwandet | 174,298,200 |
| 2 | Madarasa manne Mwandet sekondari | Mwandet | 88,552,500 |
| 3 | Kiwanda cha vifungashio aina ya mabox-Kisongo [Active Packeging] | Kisongo | 950,000,000 |
| 4 | Kivuko Kata ya Moivo | Moivo | 34,400,000 |

**B. Mradi uliyowekwa Jiwe la Msingi**

| Na | Mradi | Kata | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa maji Kitongoji cha Ekenywa | Olturument | 58,448,099.45 |

**C. Miradi ya iliyofunguliwa yenye thamani shilingi 330,201,600**

| Na | Mradi | Kata | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Kituo cha Afya Engorora | Kisongo | 151,501,600 |
| 2 | Mradi wa Shamba la Samaki Trust Patrick | Olorien | 178,700,000 |

Gharama za miradi hiyo imetokana na michango kama ifuatavyo;-

| Nguvu za Wananchi | Halmashauri | Serikali Kuu | Wadau wa Maendeleo |
|---|---|---|---|
| 163,350,700.00 | 80,849,699.45 | 255,000,000.00 | 1,136,700,000.00 |

**Mheshimiwa Rais,**

Katika mwaka **2016** wananchi walichanga shilingi **25,066,700** na mwaka **2017** shilingi **27,215,800**. Huu ni mchanganuo wa matumizi kwa mwaka 2016

| Na | Mwaka | Kiasi | Matumizi | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2016 | **25,066,700.00** | Shughuli ya Mwenge | 20,509,456 |
| | | | Miradi ya Maendeleo | 3,500,000 |
| | | | Salio | 1,057,244 |

**Mheshimiwa Rais,**

Kuhusu "**MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI**" chini ya kauli mbiu "***Tanzania bila ya maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI; inawezekana ifikapo mwaka 2030"*** Halmashauri ina vituo 52 vya huduma za afya pamoja na upimaji wa UKIMWI/VVU. Elimu juu ya ugonjwa huo imetolewa kwa wananchi kupitia mabaraza **25**, Vijana wa bodaboda **206**, Mtandao wa wanawake wafanyabiashara **88** nk. Kwa mwaka **2016/2017** watu **39,379** (Me **16,985** na Ke **22,394**) walijitokeza kupima. Waliogundulika kuwa na maambukizi ni **1,062** (Me **439** na Ke **623**). Hali ya maambukizi katika Halmashauri ya Arusha kwa ujumla ni **2.7%**.

**Mheshimiwa Rais,**

Kuhusu "**MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA"** chini ya kauli mbiu **"*Shiriki kutokomeza malaria kabisa kwa manufaa ya jamii"*** elimu ya kujikinga na Malaria inatolewa kwa ukamilifu kwa kushirikiana na wadau wetu. Maambukizi ya Malaria yamepungua kutoka **0.4%** mwaka 2015/2016 hadi **0.3%** mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Rais,**

Kuhusu **MAPAMBANO DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA,** chini ya kauli mbiu ya ***"Tuwajali na tuwasikilize watoto na vijana"*** elimu imetolewa katika Vijiji. Halmashauri inawasaidia walioathirika na madawa ya kulevya kwa kupitia Hospitali ya Olturumet na Zahanati ya Ester. Aidha, Halmashauri kushirikiana na vyombo vya usalama vilifanya "Operation" katika maeneo ya

Lemanyata, Olkokola, Losinoni juu, Oldonyowas. Magunia **612** ya bangi yalikamatwa na mashamba **8** ya bangi yenye ukubwa wa hekari **1** kila moja yalifyekwa na kuteketezwa kwa kuchomwa moto, na Watuhumiwa 30 walikamatwa kwa nyakati tofauti na kufikishwa mahakamani.

**Mheshimiwa Rais,**

Kuhusu "**MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA**" na athari zake chini ya kauli mbiu ***"Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo, amani na usalama wa Taifa letu"***. Halmashauri kupitia TAKUKURU Wilaya imeendelea na jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa, kukemea, kuelimisha jamii kutojihusisha na rushwa. Mwaka 2016/17 elimu juu ya rushwa ilitolewa, vilabu **22** vya Rushwa vilifunguliwa katika shule za Sekondari, kimoja katika Chuo, **3** shule za Msingi, mikutano **36** ya hadhara, semina **26**, uandishi wa makala **2**, na maonyesho **2** yamefanyika, machapisho **450** yamegawiwa na jumla ya taarifa **76** zenye tuhuma mbalimbali zimepokelewa. Majalada **55** yalifunguliwa, **11** yalifungwa kwa kutokuwa na ushahidi. Jumla ya kesi 5 za rushwa zinaendelea Mahakamani. TAKUKURU imepanua wigo wa kusogeza huduma kwa wananchi kupitia simu ya bure ya dharura nambari **113**.

**Mheshimiwa Rais,**

Sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha tunawatakia afya njema wakimbiza Mwenge kitaifa na safari njema, Mungu awalinde katika kazi yenu ili mtimize jukumu mlilopewa la kukimbiza mwenge wa Uhuru na kutoa ujumbe wake hadi mwisho wa safari kwa amani na salama.

Ahsante sana, ni sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

**Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee**!

Alexander Mnyeti
**MKUU WA WILAYA ARUMERU**

## TARIFA FUPI YA MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU
## 4 SEPTEMBA 2017

Mimi **Dkt. Wilson Mahera Charles**, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, ninayofuraha kuukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, leo tarehe **4 Septemba 2017** ukiwa unawaka, unameremeta ikiwa ni pamoja na wakimbiza Mwenge Kiwilaya, Kimkoa na Kitaifa wote wakiwa salama na afya njema kutokana na matunzo mazuri waliyoyapata katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha

Aidha, kwa upendeleo wa kipekee nitawataja kwa majina wakimbiza Mwenge Kimkoa na Kitaifa. Wakimbiza Mwenge Kimkoa nao ni; Ndugu **Marengo William**, **Joseph Losioki Lukumay**, **Clinto P. Msechu**, na **Ignas Kassim.**

Wakimbiza Mwenge Kitaifa ni **Salome Obadia Mwakitalima**, **Shukran Islam Msuri**, **Frederick Joseph Ndahani**, **Vatima Yunus Hassan**, **Bahati Mwaniguta Lugodisha** na mwisho ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa **Ndugu, Amour Hamad Amour**.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha Mwenge huu wa Uhuru umekimbizwa Kilometa **88** na kukagua na kufungua miradi yenye thamani ya Shilingi **1,635,900,399.45** katika Sekta za Maji, Elimu, Afya, Viwanda na Uvuvi. Aidha, jumla ya shilingi **100,000,000** imetolewa kwa vikundi ili kuwezesha wananchi kiuchumi.

**Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!!!**

Dkt. Wilson Mahera Charles
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**

*Kiambatanisho "A"*

## ORODHA YA VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOPEWA MKOPO

## MWAKA 2014/2015

| NA | JINA LA KIKUNDI | IDADI YA WANACHAMA | SHUGHULI ZAO | KIASI CHA MKOPO | MKOPO NA RIBA | MAREJESHO | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ENYORATA Y GROUP | 28 | Kilimo na ufugaji | 1,800,000 | 1,980,000 | 1,980,000 | 0 |
| 2 | EMAYAN Y GROUP | 43 | Kilimo na Ufugaji | 2,500,000 | 2,750,000 | 2,750,000 | 0 |
| 3 | RATAENYO Y GROUP | 20 | Kilimo na Ufugaji | 1,500,000 | 1,650,000 | 1,650,000 | 0 |
| 4 | MURETE Y GROUP | 10 | Kilimo na Ufugaji | 1,500,000 | 1,650,000 | 1,650,000 | 0 |
| 5 | MALAKO Y GROUP | 12 | Kilimo na Ufugaji | 1,500,000 | 1,650,000 | 1,650,000 | 0 |
| 6 | ARUSHA DC VIJANA SACCOS | 60 | Kuweka Hisa | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| | **JUMLA** | **173** | | **9,300,000** | **10,230,000** | **10,230,000** | **0** |

*Kiambatanisho "B"*

**VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOPEWA MKOPO**

**MWAKA 2015/2016**

| NA | JINA LA KIKUNDI | IDADI YA WANACHAM A | SHUGHULI ZAO | KIASI CHA MKOPO | MKOPO NA RIBA | MAREJESH O | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MELIARA Y GROUP | 5 | Kilimo cha Mbogamboga | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 2 | MWANDET Y GROUP | 20 | Ufugaji | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 3 | TONYWA Y GROUP | 22 | Ufugaji | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 4 | EENYUNOTO Y GROUP | 35 | Unenpeshaji wa Kondoo | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 5 | LEMONG'O Y GROUP | 5 | Kilimo | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 6 | IGWE Y GROUP | 33 | Kilimo | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 7 | ORANGAI Y GROUP | 5 | Kilimo | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 8 | OLDONYOSAMBU WORKSHOP | 5 | Seremala | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 9 | NASIOKII Y GROUP | 19 | Kilimo na Ufugaji | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| | **JUMLA** | **170** | | **18,000,000** | **19,800,000** | **19,800,000** | 0 |

*Kiambatanisho “C”*

## VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOPEWA MKOPO

## MWAKA 2016/2017

| NA | JINA LA KIKUNDI | IDADI YA WANA CHAMA | SHUGHULI ZAO | TAREHE YA KUPEWA MKOPO | KIASI CHA MKOPO WALICHOPATA | MKOPO NA RIBA | MAREJESHO | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Umoja Youth Group | 11 | Kuchomelea “Welding” | 26/8/2016 | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | 0 |
| 2 | Eung’ani Youth Group | 19 | Ufugaji | 26/8/2016 | 3,000,000 | 3,300,000 | 3,300,000 | 0 |
| 3 | Kiranyi Meru Youth Group | 10 | Uchapishaji | 26/8/2016 | 3,000,000 | 3,300,000 | 1,325,000 | 1,975,000 |
| 4 | Emayani destiny Youth Group | 8 | Hisa na Biashara ya Mazao | 26/8/2016 | 3,000,000 | 3,300,000 | 3,300,000 | 0 |
| 5 | Twayo Youth Group | 16 | Hisa na Kilimo cha Mboga | 26/8/2016 | 3,000,000 | 3,300,000 | 3,300,000 | 0 |
| 6 | Kiranyi Youth Group | 15 | Kutengeneza shanga na viatu vya kimasai | 26/8/2016 | 3,000,000 | 3,300,000 | 2,530,000 | 770,000 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Fajomelo Youth Group | 5 | Biashara ya Mazao | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 2,007,000 | 743,000 |
| 8 | Mirongoine Youth Group | 6 | Kuweka Hisa | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 1,931,400 | 818,600 |
| 9 | Mashiva Youth Group | 5 | Biashara na kuweka Hisa | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 2,246,700 | 503,300 |
| 10 | Gepph Youth Group | 5 | Biashara ya chakula | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 1,471,200 | 1,278,000 |
| 11 | Bloga Youth Group | 5 | Biashara ya mazao na kuweka hisa | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 1,840,000 | 910,000 |
| 12 | ASODEG Youth Group | 26 | Kuweka hisa na tenda za usafi | 10/11/2016 | 3,000,000 | 3,300,300 | 2,475,000 | 825,000 |
| 13 | Kimunyaki Esivata group | 6 | Biashara ya Duka | 10/11/2016 | 2,500,000 | 2,750,000 | 2,070,000 | 680,000 |
| 14 | Embijani madukani Group | 9 | Biashara ya Duka | 1/2/2017 | 3,000,000 | 3,300,000 | 1,650,000 | 1,650,000 |
| 15 | Uunguni Youth Group | 11 | Kufyatua Matofali | 1/2/2017 | 3,000,000 | 3,300,000 | 1,905,000 | 1,395,000 |
| 16 | Enyorata Youth Group | 6 | Ufugaji | 1/2/2017 | 3,000,000 | 3,300,000 | 1,650,000 | 1,650,000 |
| | **JUMLA** | **154** | | | **44,000,000** | **48,400,000** | **35,202,100** | **13,197,900** |

*Kiambatanisho "D"*

**ORODHA YA VIKUNDI VYA VIJANA VINAVYOPATA MKOPO MWAKA 2017/2018 AWAMU YA KWANZA**

| NA | JINA LA KIKUNDI | IDADI YA WANANCHAM | SHUGHULI ZAO | KIJIJI | KATA | NAMBA YA AKAUNT | KIASI CHA MKOPO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Melikizedeki Group | 6 | Ufugaji wa Ng'ombe | Likamba | Musa | 42110008086-NMB | 5,000,000 |
| 2 | Eng'ilang'et Y Group | 5 | Ufugaji wa Kuku na Ng'ombe | Sekei | Kiutu | 42110006200-NMB | 3,000,000 |
| 3 | Enjoloto Group | 5 | Kilimo cha viazi na mbogamboga | Sekei | Sokoni II | 152270694200-CRDB | 4,500,000 |
| 4 | Endeves Y. Group | 7 | Saluni ya kiume na Karakana | Mbuyuni | Oljoro | 40810055004-NMB | 5,000,000 |
| 5 | Umoja Youth Group | 6 | Kuchomelea "Welding" | Ilkilorit | Moivo | 40810043139-NMB | 6,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Meliara Youth Group | 5 | Kilimo cha Mbogambog a | Midawe | Bangata | 42110006200-NMB | 5,000,000 |
| 7 | Endubulu | 12 | Ufugaji na Kilimo | Kivululu | Oltroto | 152271852900-CRDB | 4,500,000 |
| | **JUMLA** | **46** | | | | | **33,000,000** |

**ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE VINAVYOPATA MKOPO MWAKA 2017/2018 AWAMU YA KWANZA**

| NA | JINA LA KIKUNDI | IDADI YA WANACHAMA | SHUGHULI ZAO | KIJIJI | KATA | NAMBA YA AKAUNTI | KIASI CHA MKOPO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Emainyo Group | 20 | Mashine ya kusaga na biashara ya mazao | Oldonyowas | Oldonyowas | 021030100671-MERU COM.BANK | 5,000,000 |
| 2 | Nabulaa Group | 16 | Ufugaji wa Kondoo | Olchorovos | Musa | 0152268867100-CRDB | 5,000,000 |
| 3 | Kolimba Juhudi Group | 14 | Biashara ya mazao na mashine ya kusaga nafaka | Olovolos | Kimunyaki | 43910000731 NMB | 4,000,000 |
| 4 | Indiandumi Group | 5 | Mapishi | Mringa | Olorieni | 0152275485200-CRDB | 4,000,000 |
| 5 | Byera Group | 5 | Ufugaji wa Nguruwe | Mringa | Olorien | 43910001287-NMB | 5,000,000 |
| 6 | Matimu Group | 30 | Kuweka hisa na Ufugaji wa Kondoo | lemanyata | Lemanyata | 42710016246 NMB | 4,000,000 |
| 7 | Natasyeko Group | 6 | Biashara | Lengijave | Olkokola | 42110006591-NMB | 4,000,000 |
| 8 | Ewong’an Group | 10 | Ufugaji wa Kondoo | Lengijave | Olkokola | 42110006590-NMB | 5,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Urakozi Group | 5 | Mapishi na Upambaji | Seuri | Otrument | 0152270693200-CRDB | 5,000,000 |
| 10 | Elotiengai Group | 10 | Kuweka hisa Ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga | Osunyai | Oltroto | 0152270694000-CRDB | 3,000,000 |
| 11 | Matingidata Group | 10 | Kuweka hisa, Ufugaji wa kuku na kilimo cha mbogamboga | Osunyai | Oltroto | 0152270692700-CRDB | 3,000,000 |
| 12 | Kinoto Group | 20 | Utengenezaji wa unga wa lishe, kuweka hisa, Mapishi na Upambaji | Saitabau | Tarakwa | 42710015100-NMB | 4,000,000 |
| 13 | Nasaruni Group | 30 | Kuweka hisa na biashara ya mazao | Oloitushula | Musa | 40810053624-NMB | 4,000,000 |
| 14 | Lolovoni group | 30 | Kuweka hisa na ufugaji | Oloitushula | Musa | 40810047303-NMB | 4,000,000 |
| 15 | Onyange W. Group | 5 | Biashara ya mazao | Ngaramtoni | Olmotonyi | 42710015992-NMB | 3,000,000 |
| 16 | Mbieshisia W.Group | 8 | Mapishi | Emaoi | Olmotonyi | 42710012539-NMB | 5,000,000 |
| | **JUMLA** | **224** | | | | | **67,000,000** |

*Kiambatanisho "F"*

**MUHTASARI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017**

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI/KATA | TUKIO | GHARAMA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa maji Ekenywa | Oltrument | Kuweka jiwe la msingi | 58,448,099.45 |
| 2 | Bweni Kidato cha 5 & 6 Mwandet Sekondari | Mwandet | Kuzindua | 174,298,200.00 |
| 3 | Madarasa manne Mwandet Sekondari | Mwandet | Kuzindua | 88,552,500.00 |
| 4 | Kituo cha Afya Engorora | Kisongo | Kufungua | 151,501,600.00 |
| 5 | Kiwanda cha vifungashio | Kisongo | Kuzindua | 950,000,000.00 |
| 6 | Mradi wa ufugaji samaki | Olorieni | Kufungua | 178,700,000.00 |
| 7 | Kivuko | Moivo | Kuzindua | 34,400,000.00 |
| | | | **JUMLA KUU** | **1,635,900,399.45** |

*Kiambatanisho "G"*

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU**

**MWAKA 2016**

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI/KATA | TUKIO | HALI YA SASA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Ofisi ya Kijiji-Sasi | Bangata | Ufunguzi | Ofisi inatumika |
| 2 | Mradi wa kilimo cha mboga mboga-Kikundi cha Vijana Meriara | Bangata | Kutembelea na Kukagua kazi za kikundi cha Vijana Meriara | Kikundi kinaendelea |
| 3 | Mradi wa Bweni la wanafunzi-Sekondari ya wasichana Sakura | Bangata | Uzinduzi | Bweni linatumika |
| 4 | Mradi wa kuuza Samani- New World Furniture Ngaramtoni | Ngaramtoni | Uzinduzi | Mradi unaendelea |
| 5 | Mradi wa Barabara ya Mahakama ya Afrika (African Tribunal) | Mateves | Ufunguzi | Barabara inatumika |
| 6 | Mradi wa Kituo cha Afya-Engorora | Kijiji cha Engorora | Jiwe la Msingi | Mradi umezinduliwa na Mwenge wa Uhuru 2017 na utaanza kutoa huduma. |
| 7 | Mradi wa Maji Likamba | Kijiji cha Likamba | Jiwe la Msingi | Mradi unaendelea kutekelezwa |

*Kiambatanisho "H"*

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU**

**MWAKA 2015**

| NA | JINA LA MRADI | SEHEMU/KATA | TUKIO | HALI YA SASA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Daraja la Engorola Barabara Kisongo-Musa-Olchorovus | Kisongo | Ufunguzi | Daraja linatumika |
| 2 | Ujenzi wa Mradi wa Maji | Kiranyi | Uzinduzi | Unatumika |
| 3 | Shamba Darasa la Samaki na | Makao makuu ya Halmashauri | Uzinduzi | Linatoa huduma |
| 4 | Uendelezaji wa Bustani ya Miche ya Miti | Makao makuu ya Halmashauri | Kutembelea na kukagua | Linatoa huduma |
| 5 | Ujenzi wa Jengo la-OPD Kito cha Afya Oldonyosambu | Oldonyosambu | Uzinduzi | Kinatuoa huduma |
| 6 | Ujenzi wa Maabara 3 za sayansi Shule ya Sekondari Lengijave | Olkokola | Ufunguzi | Zinatumika |
| 7 | Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu Shule ya Msingi Ilboru | Moivo | Uzinduzi | Bweni linatumika |
| 8 | Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa Shule ya Msingi Ilboru | Moivo | Ukaguzi | Madarasa yanatumika |
| 9 | Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Lovilukuny | Kisongo | Jiwe la Msingi | Ofisi inatumika |

*Kiambatanisho "I"*

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU**

**MWAKA 2014**

| NA | JINA LA MRADI | SEHEMU/KATA | TUKIO | HALI YA SASA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa maabara (2 in 1) shule ya Sekondari Mlangarini. | Mlangarini | Jiwe la Msingi | Mradi unaendelea vema, unatoa huduma. |
| 2 | Ujenzi wa kituo cha Afya Nduruma | Nduruma | Ufunguzi | Kituo kinatoa huduma |
| 3 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa-shule ya sekondari Mringa | Olorieni | Ufunguzi | Madarasa yanatumika. |

***Angalizo:***
*Mwaka 2014 Mbio za Mwenge wa Uhuru ilifanyika kiwilaya hivyo Miradi iligawanywa kwa upande wa Halmashauri ya Arusha na Meru.*

**SHUKRANI**

Shukrani za dhati kabisa ziwaendee **Wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha** kwa ushirikiano wao katika kuchangia, kuupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru mwaka 2017.

**Wadau wote wa Maendeleo** katika Halmashauri ya Arusha kwa kujitoa kwao kushiriki na kukubali kuupokea Mwenge wa Uhuru, ni fahari iliyo njema na ya kujivunia kushiriki maendeleo kwa umoja.

**Kamati zote za Mwenge**, Kamati ya Uhamasishaji/Ushehereshaji, Chakula, Risala na Taarifa, Ulinzi na Usalama, Usafiri na Ujenzi. Tunawashukuru Wajumbe wote wa kamati kwa umoja wao na kujitoa kwao kuhakikisha Mwenge wa Uhuru unakirimiwa na kufanikiwa pasipo na dosari yoyote.

**Waheshimiwa Madiwani** wakiongozwa na Mwenyekiti **Mheshimiwa Noah Sapuk** kwa ushiriki wao wa kuukimbiza Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri yetu ya Arusha.

**Wakuu wa Idara na vitengo, Watendaji wote wa Kata na Vijiji** kwa kujitoa kwao katika kuhakikisha Mwenge wa Uhuru unafanikiwa katika Halmashauri yetu. Afisa Vijana **Ndugu Ahadi Mlay** (Mratibu wa mbio za Mwenge wa Uhuru) kwa uratibu wa karibu wa kufanikisha mbio za Mwenge wa Uhuru. Idara ya Mipango ikiongozwa na **Ndugu Nhojo Allan Kushoka** akishirikiana na **Ndugu Innocent H. Mariki** kwa kuandaa na kuratibu taarifa zote za miradi na mpangilio wa Kijitabu hiki cha Mbio za Mwenge wa Uhuru **Septemba, 3 Mwaka 2017**.

**Mwenyekiti wa Kamati** ya Mwenge ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Arumeru **Ndugu Alexander Pastory Mnyeti** pamoja na kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa kufanikisha kufanyika kwa mbio hizi kwa usalama na utulivu.

Mwisho kabisa, shukrani za dhati ziende ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha chini ya uongozi wa **Ndugu Mrisho Mashaka Gambo** kwa ushauri na ushiriki wao katika kufanikisha Mbio hizi za Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri yetu.

Si rahisi kuwataja kwa majina wote walioshiriki kufanikisha mbio hizi, ila michango yao ni ya thamani sana kwetu.

**ASANTENI SANA NA MUNGU AWABARIKI.**

Dkt. Wilson Mahera Charles (PhD)
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI WILAYA YA ARUSHA**